SCHOOL BASED ASSESSMENT

KISWAHILI
SEHEMU B

(For Regular Learners and Learners with Physical Disability)

Gredi ya 4 - 2023

JINA LA MWANAFUNZI : _____GREDI : _____

NAMBARI YA TATHMINI:_____

TAREHE:_____

JINA LA SHULE: _____

KWA MATUMIZI YA MTAHINI

JEDWALI LA ALAMA

	ZOEZI LA 3 UFAHAMU WA KUSOMA	ZOEZI LA 4 SARUFI	ZOEZI LA 5 KUANDIKA
Swali	**1-16**	**17-30**	**31**
Upeo	**16**	**14**	**10**
Alama za mwanafunzi			
Kiwango Cha Utendaji			

Tathmini hii ina kurasa 10 zilizopigwa chapa.

Geuza ukurasa

©2023 The Kenya National Examinations Council

ZOEZI 3: UFAHAMU WA KUSOMA

Swali la 1 hadi la 4
Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.

Vifaa vya kidijitali vina manufaa mengi hasa katika ujifunzaji. Vifaa hivi vimefanya masomo kuwa rahisi. Unaweza kufanya shughuli nyingi za ujifunzaji ukiwa ndani au nje ya darasa.

Nina hakika kuwa umewahi kutumia rununu au kinasasauti kujifunza. Ni rahisi kujifunza matamshi bora kwenye vifaa hivi. Unasikiliza tu mwalimu anavyotamka. Nawe unatamka hivyo hivyo. Wewe pia unaweza kuwasaidia wenzako kujifunza kupitia vifaa hivi. Unaweza kutumia rununu ya mzazi au mlezi wako kujirekodi ukikariri shairi kuhusu bidii. Unaweza kuwatumia wenzako shairi hilo mtandaoni. Vilevile, mnaweza kulisikiliza shairi hilo darasani pamoja. Hapo utakuwa umemfunza mwalimu pamoja na wenzako. Wakati huo huo, wenzako wanaweza kutoa maoni kuhusu shairi lako. Nawe pia utakuwa umejifunza.

Ni muhimu kuwa na nidhamu unapotumia vifaa vya kidijitali. Uvitumie tu wakati unaofaa. Unapopewa ruhusa ya kuvitumia, **vitunze** visiharibike. **La muhimu zaidi ni kutumia mitandao salama kila unapojifunza.**

1. Unaweza kujifunza ukiwa_____ya darasa.

2. Katika kifungu, mzazi au mlezi anamsaidia mtoto kujifunza. Anamsaidia vipi?

   _____

3. **La muhimu zaidi ni kutumia mitandao salama kila unapojifunza.** Unafikiri utapata hasara gani usipotumia mitandao salama?

   _____

4. Kulingana na kifungu, maana ya neno **vitunze** ni:

   _____

 ©2023 The Kenya National Examinations Council

Swali la 5 hadi la 8

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.

Mama safi ni mfanyabiashara maarufu katika Soko la Jikaze. Mama huyu anajulikana kwa bidii na usafi wake. Yeye huamka asubuhi na mapema kuelekea sokoni kuuza bidhaa. Kibanda chake kina mahindi, maharagwe, mboga na matunda mbalimbali.

Kibanda cha Mama Safi kinawavutia wateja wengi. Hao huvutiwa na usafi kwenye kibanda hicho. Mama Safi hufagia kibanda chake na kuokota taka kila siku. Ana pipa maalum ambapo anatupa taka hizo. Yeye huwashauri wateja wake kutupa maganda ya matunda hapo.

Hakika bidii na usafi wa Mama Safi umemletea faida nyingi. Pato lake limeongezeka. Sasa anaweza kuilisha vyema familia yake. Watoto wake wana mavazi bora na wanasoma vyema. Wafanyabiashara wengine wamejifunza mengi kutoka kwake. **Siku hizi wao hufika kazini mapema.** Pia, huwezi kuona taka yoyote katika vibanda vyao. Soko la Jikaze limekuwa safi ajabu.

5. Mama Safi anafanya kazi wapi?

   _____

6. Mama Safi analinda mazingira kwa vile:

   _____

7. Sentensi**, siku hizi wao hufika kazini mapema** imetumiwa katika kifungu. Inaonyesha kuwa wafanyabiashara ni wenye :

bidii	nguvu	utiifu	furaha

   _____

8. Umeenda kwa kibanda cha Mama Safi. Unadhani utapata matunda gani?

   _____

 ©2023 The Kenya National Examinations Council

Swali la 9 hadi la 12

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.

Musa alishangaa kumwona kuku kitandani. Alisogea karibu na kumtazama. Kuku alidhani Musa alitaka kumfukuza. Alianza kuteta huku akimtazama Musa.

Baba yake Musa alisikia sauti kubwa ya kuku. Alikwenda mbio kumwangalia. Alipofika alimwona Musa akimtazama kuku kwa huruma. Baba alimshika Musa begani.

“Kuna nini? Unamwogopa? Hana neno huyu. Acha tumtoe kitandani.” Baba alisema. Baba alimtoa kuku kitandani.

“Kuna yai! Baba, kuku wetu ametaga.” Musa alisema kwa furaha.

“Sasa umejua kwa nini kuku alikuwa anateta. Alikuwa analinda yai lake.” Baba alisema huku akitabasamu.

“Nitamtengenezea mahali pazuri pa kutagia mayai.” Musa alisema kisha akachukua boksi dogo na kulitia nyasi nyepesi. Alitia changarawe kidogo kwenye boksi hilo. Alilipeleka boksi kwenye kizimba cha kuku. Alitia yai kwenye boksi hilo. Baadaye alimtafuta kuku ili amwonyeshe mahali salama pa kutagia. Alimkuta kuku nyuma ya nyumba. Alimtupia mahindi. Kuku alimfuata huku akidona mahindi hayo. Mwishowe walifika kwenye kizimba. Kuku aliingia haraka naye Musa akafunga kizimba.

9. Kwa nini kuku aliteta alipomwona Musa?

_____

 ©2023 The Kenya National Examinations Council

10. Baba anamwambia Musa kuwa kuku hana neno ili _____Musa.

amtulize	amshauri

_____

11. Musa anamjali kuku kwa sababu:

_____

12. Kifungu kinaonyesha njia za kumtunza kuku. Andika njia nyingine moja ambayo Musa na babake wangetumia kumtunza kuku wao.

_____

Swali la 13 hadi la 16

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.

Karibu kiti kalia, mezani we karibia,

Chakula nimeandaa, tuleni na tunywe pia,

Shukrani tunatoa, kwa Mungu kutujalia,

Chakula ukipakua, nidhamu kumbuka pia.

Chakula unapotia, kiwe kiasi sikia,

Sijaze kupindukia, sahani utachafua

Ukila kikipungua, unaweza kurudia,

Lishe ukaongezea, tosha yako kufikia.

Chakula chako fungia, kinywani unapotia,

Si vizuri **kuongea**, na kinywa kukifungua,

Chakula kitapotea, kipitie kwenye pua,

Utabaki ukilia, chakula chakupalia.

 ©2023 The Kenya National Examinations Council

Leo ninakwambia, hili likumbuke pia,

Sahani mezani toa, meza ipanguse pia,

Ni nzuri sana tabia, usafi kuzingatia,

Kisha asante kutoa, kwa aliyekupikia.

13. Katika ubeti wa kwanza mshairi anamkaribisha msomaji wafanye nini?

_____

14. Ubeti wa pili unakushauri uwe na tabia gani?

_____

15. Mtu akiendelea kula kupindukia ataweza kupata hasara gani?

_____

16. Badala ya mshairi kutumia neno **kuongea** angetumia:

_____

ZOEZI 4: MATUMIZI YA LUGHA

17. Kadi zifuatazo zina nomino. Chagua kadi yenye nomino ya ngeli ya **LI-YA.**

A. ndoo

B. jicho

C. ukuta

©2023 The Kenya National Examinations Council

18. Tazama picha hii:

John anasoma kitabu

Tande _____kiti rangi.

19. Tumia kiambishi kinachofaa kujaza nafasi. Zingatia mfano huu:

Mfuko wa Dani **u**napendeza.

Chumba chetu __na pazia safi.

_____

20. Chagua jibu sahihi kujaza nafasi.

Katila anatembea _____ (taratibu, wema)

21. Chagua neno linalofaa kujaza nafasi.

Kwinto_____ Salma watasoma hadithi darasani. (kwa, na)

22. Verona aliwaona ndege mtini akasema: **Ndege hawa wanapendeza**. Je, Verona angemwona ndege mmoja angesema:

_____

23. Umefua shati la kaka yako mdogo. Chagua kitenzi kinachofaa kujaza nafasi.

Wewe _____kaka yako mdogo shati.

(umefuliwa, umemfulia)

©2023 The Kenya National Examinations Council

24. Fuata mfano wa A kujaza nafasi katika B.



_____

25. **"Huree!** Timu yetu imeshinda." Maria alisema.

Neno **Huree!** linaonyesha _____.(tumaini, furaha, mshangao)

26. Kuna maneno yanayokaribiana kimatamshi kama vile **damu --- tamu**. Andika neno linalokaribiana kimatamshi na neno **bata**.

_____

27. Linda anataka kwenda kucheza. Linda _____ kabla ya kutoka.

(atafanya haki, atapiga hodi, ataomba ruhusa)

28. Jordan alimwona ndovu mbugani. Jina lingine la ndovu ni_____.

29. Badala ya kusema, Bamuda ameenda chooni tunasema, Bamuda ameenda msalani. Badala ya kusema, Mama Asha ana mimba tutasema, Mama Asha ni: (mkazamwana, mjamzito)

_____

30. Mwenzako ana tabia ya kutozingatia maagizo ya walezi na walimu. Utatumia methali gani kumshauri aache tabia hiyo?

_____

©2023 The Kenya National Examinations Council

ZOEZI 5: KUANDIKA

31. Andika insha kuhusu:

ZIARA KATIKA MBUGA YA WANYAMA

Katika insha yako, zingatia yafuatayo:

i. Siku ya ziara
ii. Safari ya kuelekea mbugani
iii. Mambo yaliyotendeka mbugani
iv. Jambo ambalo unalikumbuka zaidi
v. Safari ya kurudi shuleni

 ©2023 The Kenya National Examinations Council

HUU NDIO UKURASA WA MWISHO ULIOPIGWA CHAPA.

©2023 The Kenya National Examinations Council